

TANGAZO

Afisa Mwandikishaji wa Jimbo la Tabora Mjini anawatangazia wakazi wote wa Manispaa ya Tabora kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha zoezi la uwekaji wazi wa Daftari la awali la Wapiga Kura kwa awamu ya pili, zoezi hili litafanyika kwa muda wa **siku 4** kuanzia tarehe **17/06/2020** hadi tarehe **20/06/2020**. Daftari litabandikwa katika **vituo vyote** vilivyotumika katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambavyo viko katika maeneo ya **Mitaa na Vijiji** katika kata husika.

Mpiga kura atakaye hakiki taarifa zake katika kituo **alichojiandikisha kilichopo katika Mtaa na Kijiji husika na akakuta taarifa zake zimekosewa** atatakiwa kufika ofisi ya **Kata ya Chemchem (Sanamu ya Mwalimu Nyerere)** ambapo mashine (**BVR KIT**) moja itawekwa kwa ajili ya Uboreshaji wa Taarifa.

KUMBUKA zoezi hili **halitahusisha:-**

1. Kuandikisha Wapiga Kura **wapya**
2. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura waliopoteza au kadi zao kuharibika
3. Kuhamisha taarifa za wapiga kura waliohama kata au Jimbo.


Bali Litahusisha

4. kurekebisha taarifa binafsi za Mpiga Kura zilizokosewa mfano majina, umri, jinsi miaka nk.
5. Kufuta taarifa za Mpiga kura aliyekosa sifa mfano waliofariki.
6. Kuweka pingamizi dhidi ya mpiga kura aiyejiandikisha asiye na sifa.

MUHIMU

Sifa muhimu ya kupiga kura siku ya Uchaguzi Mkuu ni kuwa na Kadi ya Mpiga Kura.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:


Bosco O. Ndunguru
AFISA MWANDIKISHAJI
JIMBO LA TABORA MJINI

AFISA MWANDIKISHAJI
JIMBO LA
TABORA MJINI